RÉPUBLIQUE FRANÇAISE
Liberté
Égalité
Fraternité

INSP
Institut national du service public

Concours d'entrée 2025

Voie Orient

Concours externe

Section : Afrique

Langue : Swahili

5ème épreuve d'admissibilité

Une épreuve consistant en des réponses courtes, dans la langue choisie au moment de l'inscription, à des questions à partir d'un dossier dans cette même langue permettant d'apprécier les connaissances linguistiques sur les thèmes économiques, culturels, sociaux de la section géographique choisie et l'aptitude à formuler des réponses complexes.

L'usage du dictionnaire est autorisé pour cette seule épreuve en arabe littéral, chinois, haoussa, hébreu, hindi, japonais, mandingue, persan, peul, swahili, turc et wolof. Pour ces langues, tous types de dictionnaires (à l'exclusion des dictionnaires électroniques) de la langue de l'épreuve vers le français, vers l'anglais ou vers une langue tierce sont autorisés, et vice versa. Les candidats utilisant un dictionnaire de langue de l'épreuve vers une autre langue que le français et l'anglais peuvent utiliser un dictionnaire de cette langue tierce vers le français et l'anglais. Sont, en outre, autorisés les dictionnaires rédigés exclusivement dans la langue de l'épreuve. Les dictionnaires peuvent faire l'objet de contrôles durant les épreuves. Ils ne peuvent être ni annotés, ni prêtés, ni échangés entre candidats durant l'épreuve.

Toute note inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire.

Durée : 3 heures – coefficient 3

Sujet

Kwa kutumia ujuzi wako na makala zifuatazo, jibu maswali yaliyo hapa chini, kwa kiswahili.

Question n°1 : Je, sera ya biashara huria inaleta faida gani na hatari gani, kwa nchi za Afrika ?

Question n°2 : Je, kuendeleza biashara kati ya nchi za Afrika ("biashara ya kikanda") kutaleta manufaa gani kwa bara la Afrika ?

Question n°3 : Je, serikali za Afrika zinawezaje kuhakikisha kwamba biashara huria inaboresha maisha ya watu wote, wakiwemo maskini, vijana, na wanawake ?

Document 1

VOA Swahili, na Kennedy Wandera, 1 Julai 2024 *(https://www.voaswahili.com/a/7680824.html)*

Kenya na Umoja wa Ulaya kuanza kutekeleza makubaliano ya biashara huru

Waziri wa Uwekezaji, Biashara na Viwanda Bi. Rebeca Miano alitangaza Jumatatu kwamba Kenya na EU zimeanza kutekeleza Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi (EPA) unaoruhusu kuingia kwa bidhaa za kila upande katika masoko yao bila ya kutozwa ushuru. […]

Umoja wa Ulaya ni kituo cha kwanza cha mauzo ya nje cha Kenya na mshirika wa pili wa kibiashara kwa ukubwa baada ya Benki ya Dunia. Ni fursa katika mojawapo ya masoko makubwa ya nje ya Kenya ambayo inachangia asilimia 21.1 ya jumla ya mauzo ya nje ya nchi ya Kenya, yenye thamani ya dola bilioni 1.4 za Kimarekani.

Charles Karisa ambaye ni mtaalam wa biashara, uchumi na uwekezaji nchini Kenya, anaeleza kuwa sasa ni bidii ya Kenya kuhakikisha inaongeza ujazo wa bidhaa zake kwenye soko la Ulaya kuongeza ujasiriamali na uwekezaji unaotabirika kujiendeleza.

Alisema kuwa Kenya inastahili kutumia mkataba huo kuimarisha ushindani wa soko lake la mauzo ya nje na kuacha mategemeo ya chai, kahawa, maua, nguo na chuma ambazo ndizo bidhaa zake muhimu kwenye soko la nje.

Mauzo ya kiasi kikubwa ya Kenya kwa soko la Umoja wa Ulaya ni bidhaa za kilimo kama vile mboga, matunda, chai na kahawa.

Kupitia mkataba huu, wakulima wa Kenya wataongeza uwezo wa kipato na kupata uendelevu wa upanuzi wa soko linalotabirika hasa kwa samaki, mboga, matunda, maua, chai na kahawa. […]

Mkataba huo unailazimisha Kenya kuunga mkono malengo ya kimataifa ikiwa ni dhamira ya kukuza demokrasia na utawala wa kisheria, kuheshimu haki za binadamu, kuwa sehemu ya jitihada za ulimwengu za kudumisha amani na usalama na vile vile kuunga juhudi za kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa. […]

Habari za UN, na UNCTAD, 8 Disemba 2021 *(https://news.un.org/sw/story/2021/12/1133382)*

Pengo kati ya tajiri na maskini limeongezeka barani Afrika

Chini ya nusu ya nchi za Afrika ndizo zimekuwa na ukuaji wa pamoja wa uchumi katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, na hivyo kuacha asilimia 34 ya kaya katika bara hilo zikiishi chini ya mstari wa umaskini yaani dola 1.9 ya kimarekani kwa siku, utafiti mpya Kamati ya Umoja wa Mataifa ya maendeleo na biashara, UNCTAD umebainisha ukisisitiza kuwa ukuaji shirikishi haufikiki kwa nchi nyingi za Afrika. […]

Kwa mujibu wa ripoti hii mpya ya Maendeleo ya Kiuchumi ya UNCTAD ya mwaka 2021, ukuaji ambao haujawahi kushuhudiwa barani Afrika katika miaka ya 2000 haukutafsirika kuwa "maboresho makubwa katika maisha ya Waafrika wengi." Hakika, pengo la kipato kati ya matajiri na maskini limeongezeka. […]

Katibu Mkuu wa UNCTAD Rebeca Grynspan anaeleza akisema, “umaskini na ukosefu wa usawa hauepukiki. Ni zao la machaguo ya kisiasa na sera za umma. Ripoti hii itasaidia serikali za Afrika na washirika wa maendeleo kutumia vyema Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) ili kukabiliana na umaskini na ukosefu wa usawa.” […]

AfCFTA kupunguza ongezeko la umaskini na ukosefu wa usawa.

Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika, AfCFTA linaweza kuchochea ukuaji endelevu na shirikishi katika bara hili la Afrika ikiwa hatua za kusaidia wanawake, wafanyabiashara vijana na biashara ndogo ndogo zinatekelezwa.

"AfCFTA ina uwezo mkubwa wa kuchochea ukuaji wa uchumi na kubadilisha matarajio ya maendeleo ya bara kama hatua zaidi zitachukuliwa kufikia manufaa yake mengi." anasisitiza Bi. Grynspan.

Afrika Upya, Na Abebe Haile-Gabriel, Mei 2021 *(https://www.un.org/africarenewal/sw/magazine/mei-2021/kilimo-kitasaidia-au-kuzamisha-biashara-huru-ya-afrika)*

Kilimo kitasaidia au kuzamisha biashara huru ya Afrika

[…] Eneo Huru la Biashara la Bara Afrika (AfCFTA) lina uwezo wa kuinua mamilioni ya watu kutoka umaskini na kumaliza upungufu wa chakula katika Afrika. Hata hivyo, ufanisi wake unategemea uidhinishwaji na utekelezwaji, na haswa katika sekta ya kilimo.

Afrika inategemea mauzo ya bidhaa za kilimo kama kakao, kahawa, pamba, tumbaku na viungo kwa mataifa ya ulimwengu ili kupata fedha muhimu za kigeni. Lakini bara hili linaagiza vyakula muhimu kama nafaka, mafuta ya mboga, bidhaa za maziwa na nyama kwa kiasi kikubwa.

Biashara kati ya mataifa ya Afrika katika bidhaa za kilimo kama asilimia ya jumla ya biashara ya Afrika ya kilimo imesalia chini ya asilimia 20 kwa muda mrefu, moja kati ya idadi ya chini kabisa katika kanda yoyote ile. Jumla ya biashara kati ya mataifa ya Afrika ilikuwa asilimia 2 pekee katika kipindi 2015–2017, ikilinganishwa na asilimia 67 kwa biashara kati ya mataifa ya Ulaya, asilimia 61 kwa mataifa ya Asia, na asilimia 47 kwa mataifa ya mabara ya Amerika, kwa mujibu wa shirika biashara la UN la UNCTAD.

AfCFTA inakusudia kuibadilisha hali hii. Imeunda eneo huru la kibiashara lililo kubwa zaidi ulimwenguni, linalowakilisha soko la watejaa bilioni 1.2. […]

Ni katika kilimo ambako matumaini ya AfCFTA yanaweza kutimizwa. […] "Soko moja la Kiafrika lina uwezo wa kuunda mazingira bora, yenye ushindani zaidi wa biashara kwa kilimo, kuhamasisha uwekezaji zaidi na mwishowe sekta ya kilimo ya kisasa, yenye nguvu, yenye tija, inayojumuisha, na endelevu ambayo inaweza kuwaondoa mamilioni ya Waafrika kutoka kwenye umasikini". […]

Jumuiya nyingi za kiuchumi katika Afrika tayari zimetambua bidhaa za kimkakati kwa uboreshwaji zaidi […]: Afrika Mashariki imeupa kipaumbele mchele, maharagwe na bidhaa za maziwa miongoni mwa nyingine. Afrika Magharibi imeyapa kipaumbele mawele, mifugo, samaki […], miongoni mwa nyingine. Bidhaa zilizopewa kipaumbele Kusini mwa Afrika ni soya na njugu.

Mwelekeo huu wa kikanda una uwezo wa kuwajumuisha wakulima wadogowadogo ikiwa ni pamoja na wanawake na vijana […], na kuwaunganisha kwa sekta kuu ya kibinafsi inayotawala masoko ya pembejeo na mazao. […]

Afrika Upya, na Janet Edeme, Desemba 2023
(https://www.un.org/africarenewal/sw/magazine/desemba-2023/biashara-ya-ndani-ya-afrika-inatoa-fursa-kwa-ukuaji-wa-uchumi-jumuishi-na)

Biashara ya ndani ya Afrika inatoa fursa kwa ukuaji wa uchumi jumuishi na uendelevu

Usalama wa umiliki wa ardhi wa wanawake ni muhimu kwa uwezeshaji wao katika ngazi ndogo kama wazalishaji wa kilimo katika kaya na katika ngazi ya jumla kwa ajili ya kufungua manufaa ya kimageuzi, kijamii na kiuchumi. […]

Mnamo 2015, Kamati Maalumu ya Kiufundi ya AU ya Kilimo, Maendeleo Mashambani, Maji na Mazingira (STC-ARDWE) ilipitisha pendekezo lililolenga kusaidia uwezeshaji wa wanawake kiuchumi. Mataifa Wanachama yalitakiwa kubuni sera, sheria na taratibu nyingine ambazo zingeweza kuelekea kwenye ugawaji wa 30% ya ardhi iliyosajiliwa kwa wanawake. […]

Tayari, kuna mwelekeo chanya uliosajiliwa nchini Tanzania, Malawi na Uganda katika kupunguza pengo la kijinsia katika wanawake kumiliki ardhi na ushiriki wao katika uzalishaji wa kilimo. Kwa mfano, nchini Tanzania 32% ya wanawake ni wamiliki wa ardhi ikilinganishwa na 42% ya wanaume.

Hata hivyo, nchini Naijeria ni 4% tu ya wanawake, ikilinganishwa na 23% ya wanaume wanaomiliki ardhi ya kilimo. Nchini Nijer, 63% ya wanaume na 35% ya wanawake wanamiliki ardhi ya kilimo. […]

Ingawa kuna maendeleo katika baadhi ya nchi kwa utambuzi wa wazi wa haki sawa za wanawake, kukuza umiliki wa pamoja na usajili wa ardhi, kutunga sheria za kimaendeleo za urithi, ulinzi wa haki za kumiliki mali kwa wajane, bado mengi hayajafanywa. […]

Mojawapo ya malengo makuu ya Eneo Huru la Biashara la Bara Afrika (AfCFTA) ni "kukuza na kufikia maendeleo endelevu na shirikishi ya kijamii na kiuchumi, usawa wa kijinsia na mageuzi ya kimuundo ya Mataifa Wanachama".

AfCFTA inatoa fursa kwa ukuaji wa kiuchumi jumuishi wa Mataifa Wanachama ili kukuza uanuwai wa chumi na kuharakisha biashara ili kufikia uwekezaji zaidi katika kutekeleza masharti ya sheria za bara na maamuzi ambayo yanahitaji kulinda na kukuza haki za ardhi za wanawake.